

BUKU LA 10

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule ya Jimbo la Dekalb,

Jumatatu hii ijayo, nitashiriki katika mkutano wa bodi ya DCSD ambapo tutajadili hatua zinazofuata katika mipango yetu ya kurudi shule. Nitashiriki muhtasairi kutoka kwa mkutano na wewe kwa kuwa uwazi ni muhimu kwa ufanisi wetu wa kielimu. Unawezakutazama mkutano ujao wa bodi kwenye TV ya Shule za DeKalb (DSTV), Kituo 24 katika Kaunti ya DeKalb, au kwa kutembelea hapa: <https://www.dekalbschoolsga.org/communications/dstv/>.

Huku tukielekea kuwadia kufungua tena, tafadhali fahamu kwamba hakuna kitu muhimu kwangu kuliko usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wetu. Unasalia kuwa kipaumbele changu nambari moja. Ninataka pia kuwakumbusha nyinyi wote kufanya muwezavyo ili kuwa wavumilivu huku mbinu hii yetu “mpya ya kawaida” ikibadilika. Helen Keller alisema hivi, “Ijapokuwa ulimwengu huu una mateso mengi, umejawa pia na ushindi mwingi.” Ninawapongeza wanafunzi na wafanyakazi wa DCSD kwa kusalia thabiti katika janga hili lote na kuendelea mbele.

Ziara ya Divisheni ya PoPin na Uwanjani na Ofisi ya Uwajibikaji

Asante kwa Dkt. Linda Frazer na wakurugenzi kutoka idara tofauti katika Ofisi ya Uwajibikaji. Mnamo Alhamisi, nilikuwa na furaha ya kujifunza mengi kutoka kwao kuhusu kazi muhimu na msaada wanaotoa kwa wilaya yetu, ikiwemo:

- Upangaji unaondolea ambao unasababisha nafasi bunifu za kusoma kwa wanafunzi wetu.
- Kutumia data kutoka kwa tafiti na tathmini ili kutambua jinsi na wapi ambapo shule zinaweza kuimarika.
- Kushirikiana na wanafunzi na walimu kulainisha vyema matarajio ya utendakazi.

Ninataka pia kushukuru timu ya ajabu ya Shule ya Teknolojia na Mazingira ya DeKalb (DATE), ambapo nilikutana na viongozi wa Shule za Umma. Nilifurahia kuongea na washirika wote wakati wa mkutano wetu wa “kukutana na kusalimiana” huku pia nikijifunza kuhusu mambo ya kufanya ambayo wameyapanga kwa wanafunzi wetu. Lazima nitaje kwamba ushirikiano kati ya shule zetu za umma na Kituo cha Wanafunzi cha Kimataifa cha DeKalb ni wa kipekee. Ninajivunia kuhusu maendeleo ambayo Wanafunzi wetu wengi Wanaojifunza lugha ya Kiingereza (ELL) wanayafanya kwa sababu ya ushirikiano huu. Asante kwa maoni yako yanayoendelea kuhusu uzoefu wa masomo ya mtandaoni. Maoni haya ni muhimu kwangu na sisi sote katika DCSD ili kuendelea kuimarika na kufikia malengo ya juu. Ninashukuru kwa kujitolea kwako kwa ufanisi wa wanafunzi wetu.

Kuweni na wikendi njema wana-DCSD!

Shabiki wako wa #1,

Bi. Cheryl Watson-Harris, Msimamizi